Nuru ya Kiswahili, Juzuu 4(2), Desemba 2025:1-21
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru42.0121

Toni Inavyoathiri Urefu wa Irabu za Viambishi-Awali vya Nomino za Kiswahili

Pius Kiraka
Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Dodoma
pius.kiraka@udom.ac.tz

Ikisiri

Makala hii inachunguza kwa nini baadhi ya nomino za Kiswahili zina viambishi-awali vyenye irabu ndefu ilhali viambishi-awali hivyohivyo vikisikika kuwa na irabu fupi kwenye nomino zingine. Irabu ndefu za viambishi-awali si jambo geni kwenye nomino za Kiswahili. Zinaweza kusababishwa na milolongo ya konsonanti au kuungana kwa irabu. Hata hivyo, si kila irabu ndefu kwenye viambishi-awali vya nomino hutokana na michakato hiyo. Utafiti ulifanywa ili kujua sababu zingine za kutokea irabu ndefu kwenye viambishi-awali vya baadhi ya nomino za Kiswahili. Data zilikusanywa kutoka maandikoni na uwandani, zikiwa nomino zenye viambishi-awali vilivyo na irabu. Nomino hizo zilitamkwa na wasemaji wa Kiswahili wa Zanzibar. Matamshi yao yalichakatwa kwa programu ya kompyuta ili kubainisha nyakaa za irabu zinazotokea kwenye viambishi-awali. Uchanganuzi wa data uliongozwa na dhana ya urefu, urefushaji, na ufupishaji. Matokeo ya uchanganuzi yanaonyesha kuwapo kundi dogo la nomino za Kiswahili zenye viambishi-awali vyenye irabu ndefu. Inadhaniwa kuwa irabu hizo ndefu zilisababishwa na ruwaza za toni zilizokuwapo katika Mame-Bantu. Ingawa Kiswahili kimeshapoteza ruwaza za toni kilizozirithi kutoka Mame-Bantu, inadhaniwa kuwa nacho kilikuwa kikirefusha irabu za viambishi-awali vya baadhi ya nomino ili zitangamane na ruwaza za toni kwenye maumbo ya baadhi ya nomino za lugha hiyo ya kale. Kuwapo kwa nomino hizi chache zenye viambishi-awali vyenye irabu ndefu ni ushahidi mmojawapo uliobaki wa kuwapo kwa ruwaza za toni katika Kiswahili baada ya kutokea mabadiliko ya kihistoria katika lugha hii.

Dhana za Msingi: Toni, irabu ndefu, nomino, viambishi-awali, Kiswahili

Utangulizi

Kiswahili ni lugha ya Kibantu. Nomino za lugha nyingi za Kibantu zinatajwa kuwa na sehemu kuu mbili—shina la nomino na kiambishi cha nomino ambacho, kwa kawaida, ni kiambishi-awali, nacho huundwa na irabu, au konsonanti na irabu. Miongoni mwa lugha za Kibantu takribani 600 zilizochunguzwa na Heine (1982), theluthi mbili ya lugha hizo zina nomino zilizogawanywa katika makundimakundi—au ngeli za nomino—kwa kufuata viambishi-awali vinavyotokea katika nomino hizo (Katamba, 2014).

Nomino za Kiswahili nazo huundwa na kiambishi-awali na kufuatiwa na shina la nomino. Hebu chunguza nomino zifuatazo: <kichwa>, <kite>, <kiti>, <kifo>, <kisu>. Au, nomino hizi: <vichwa>, <vite>, <viti>, <vifo>, <visu>. Ukichunguza makundi hayo mawili ya nomino, utaona kuwa silabi ya kwanza ya nomino hizo, ambayo pia ndiyo kiambishi-awali cha nomino hizo, hufanana kwa kila kundi. Kiambishi-awali cha kundi la kwanza ni <ki->; na cha kundi la pili ni <vi->. Tukisikiliza kwa makini matamshi ya nomino hizo, tutagundua kuwa irabu zinazounda silabi hizo—kwenye kiambishi-awali na kwenye silabi inayofuatia, yaani kwenye shina la nomino, ni irabu fupi.

Kwa upande mwingine, hebu chunguza matamshi ya nomino zifuatazo: <kisa>, <kinu>, <kitu>. Au, matamshi ya nomino hizi: <visa>, <vita>, <vinu>, <vitu>. Tukisikiliza kwa makini matamshi ya nomino hizi, tutagundua kuwa viambishi-awali vya nomino hizi—ambavyo hufanana

kabisa na viambishi-awali tulivyoviona kwenye nomino za awali—hutamkwa kwa wakaa mrefu kuliko viambishi-awali vya nomino hizo za awali. Hili ni jambo la kustaajabisha. Je, kwa nini kiambishi-awali kilekile kiwe na irabu fupi kinapoambatana na shina fulani la nomino, ilhali kiambishi-awali hichohicho kinapoambatana na shina lingine la nomino kisikike kikiwa na irabu ndefu?

Viambishi-awali vya nomino kuwa na irabu ndefu si jambo geni katika Kiswahili. Mathalani, Steere (1943) anaeleza kuwa kiambishi-awali <wa-> kinapotokea kabla ya [shina la] neno linaloanza na irabu <e-> au <i->, irabu ya kiambishi-awali hicho huungana na irabu inayopakana nayo na kuzalisha irabu <e> iliyo ndefu k.v. <wa+izi → we:zi>. Hata hivyo, tukichunguza kwa makini maumbo ya nomino hizo zenye viambishi-awali vyenye irabu ndefu, tutaona kuwa mashina yake hayaanzi na irabu yoyote, bali huanza na konsonanti. Hivyo, irabu ndefu inayotokea kwenye viambishi-awali vyake haitokani na kuungana kwa irabu mbili. Kwa sababu hiyo, swali letu linabaki palepale: Je, kwa nini kiambishi-awali cha nomino za kundi lilelile moja kiwe na irabu fupi kwenye nomino fulani, ilhali kiambishi-awali hichohicho huwa na irabu ndefu kwenye nomino nyingine?

Kuungana kwa irabu mbili si namna pekee inayofanya viambishi-awali vya nomino za Kiswahili kuwa na irabu zinazotamkwa kwa wakaa mrefu. Kiraka (2013) anaeleza kuwa kuwapo kwa milolongo ya konsonanti halisi au milolongo ya nazali na konsonanti kwenye nomino za Kiswahili huchombeza irabu mojawapo ya neno hilo irefushwe ili kufidia irabu iliyopotea kutokana na kuwapo kwa milolongo hiyo. Pindi urefushaji huo unapofanyikia kwenye silabi ya kwanza ya nomino, silabi ambayo pia ina dhima ya kuwa kiambishi-awali cha nomino inayohusika, basi kiambishi

hicho husikika kikiwa na irabu ndefu. Chunguza matamshi ya silabi ya kwanza ya nomino zifuatazo: <kibla>, <muktadha>, <undugu>. Ukisikiliza kwa makini matamshi ya silabi zinazotokea kabla ya milolongo ya konsonanti halisi, <-bl->, <kt>, au silabi zinazotokea kabla ya milolongo ya nazali na konsonanti, <-nd->, utabaini kuwa silabi hizo zina irabu ndefu. Silabi hizo ndizo pia viambishi-awali vya nomino hizo. Nao urefu wa irabu unaotokea kwenye irabu hizo huchombezwa na milolongo ya konsonanti inayotokea baada yake. Kurefushwa kwa irabu hizo hufanywa ili kufidia irabu inayopotelea kwenye milolongo hiyo inayokiuka miundo ya asili ya silabi za maneno ya lugha za Kibantu ambazo, kwa kawaida, huundwa na konsonanti na irabu. Pamoja na ukweli huu, tunapochunguza maumbo ya nomino za Kiswahili tulizozitaja awali, zenye irabu ndefu kwenye viambishi-awali, <ki-> na <vi->, kama vile <kisa> na <vita>, tunaona kuwa nomino hizo hazina milolongo yoyote ya konsonanti halisi, wala milolongo ya nazali na konsonanti. Kwa mara nyingine tena, swali letu linabaki lilelile: Je, kwa nini kiambishi-awali cha nomino za kundi lilelile moja huwa na irabu fupi kwenye nomino fulani, ilhali kiambishi-awali hichohicho kikiwa na irabu ndefu kwenye nomino nyingine?

Inavyoonekana, kuwapo kwa viambishi-awali vya nomino vyenye irabu ndefu zisizotokana na kuungana kwa irabu, wala kuchombezwa na milolongo ya konsonanti, si jambo geni katika lugha za Kibantu. Tukichunguza kwa makini baadhi ya nomino za lugha hizo, tutaona zikiwa na maumbo yanayoelekea kufanana na yale ya nomino hizi za Kiswahili, ambapo viambishi-awali vyake vina irabu ndefu. Hebu tuangalie mifano ya nomino hizo katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Baadhi ya nomino za lugha za Kibantu zenye irabu ndefu katika viambishi-awali

Na.	Lugha	Neno				
	Kiswahili [G42]	<m**a:**ji>	<k**i:**tu>	<m**u:**wa>	<m**u:**ye>	<**u:**ki>
1	**Kihehe** [G62]		<*ik**ii**nu*>			<*uw**uu**ki*>
2	**Kishubi** [DJ64]	<*am**aa**zi*>				<*ub**uu**ki*>
3	**Kisoga** [EJ16]				<*om**uu**ka*>	
4	**Kimasaaba** [EJ31]					<*bub**uu**khi*>
5	**Kimaragoli** [EJ41]	<*am**aa**zi*>				
6	**Kitharaka** [E54]					<***uu**ki*>
7	**Kisiha** [E61]			<*m**oo**va*>		
8	**Kimachame** [E62a]			<*m**uu**wa*>		
9	**Kinyamwezi** [F22]					<*b**UU**kI*>
10	**Kinyiramba** [F31]	<*m**aa**zE*>		<*m**UU**wa*>		<***UU**kE*>
11	**Kinyaturu** [F32]				<*m**uu**ke*>	
12	**Kirungwa** [M12]					<*uw**uu**ki*>
13	**Kifipa** [M13]					<***uu**chi*>
14	**Kindengereko** [P11]					<*b**uu**si*>
15	**Kirufiji** [P12]				<*m**uu**ke*>	

Chanzo: Nurse & Philippson (1975)

Lugha nyingi za Kibantu huwakilisha sauti za irabu ndefu kwa kutumia irabu-pacha. Tukichunguza nomino za lugha hizo zilizowasilishwa hapa, tunaona kuwa kiambishi-awali cha nomino hizo kina irabu ndefu, nalo shina la nomino huanza na sauti ya konsonanti.

Ukiacha kuungana kwa irabu na milolongo ya konsonanti, hali nyingine inayodaiwa kusababisha kutokea kwa irabu ndefu kwenye viambishi-awali vya nomino katika baadhi ya lugha za Kibantu ni kuwapo kwa ruwaza fulani za toni katika lugha hizo. Mathalani, Kutsch Lojenga (2007), akichunguza mfumo wa sauti za irabu za lugha ya ishiMalila [M24], lugha izungumzwayo mkoani Mbeya, Kusini-Magharibi mwa Tanzania, alibaini

kuwa irabu za miunganiko ya viambishi-awali-vitangulizi na viambishi-awali katika nomino zinaweza kuwa ndefu au fupi, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na. 2.

Jedwali Na. 2: Irabu ndefu na fupi katika viambishi-awali-vitangulizi na viambishi-awali katika ishiMalila [M24]

Ngeli	**Irabu katika kiambishi-awali-kitangulizi na kiambishi-awali**			
	Irabu fupi	**Fasili**	**Irabu ndefu**	**Fasili**
5	<***ɪ***-*jɛ́ɛmbɛ*>	jembe	<***ií***-*fuku*>	joto
	<***í***-*joomvu*>	kivumanzi	<***íɪ***-*kʊlʊ*>	ini
	<***í***-*daadu*>	pombe ya mahindi	<***íi***-*gúle*>	kupe
	<***i***-*bumuúnda*>	bumunda	<***íi***-*βɔ*>	vita, mapigano
	<***í***-*βuututu*>	aina ya ndege	<***íɪ***-*papa*>	pafu
Kiambishi-awali-kitangulizi				
9/10	<***ín***-*haaya*>	nyumbani	<***íɪn***-*salɛ*>	chale
	<***ɪm***-*bíɪnzɔ*>	tezo	<***íɪm***-*bíla*>	mbweha
	<***ím***-*beesu*>	ukungu	<***ɪín***-*sama*>	simba
	<***i***-*futáali*>	futari	<***íɪn***-*sɪ*>	nchi, ardhi
	<***in***-*dundúulu*>	shanga za kiunoni	<***íim***-*pwa*>	moto wa nyika

Chanzo: Kutsch Lojenga (2007)

Zaidi ya hayo, katika lugha ya ekiKwaya [EJ251] na eciRuuri [EJ253], lugha zinazozungumzwa mkoani Mara, Kaskazini mwa Tanzania, irabu ndefu na irabu fupi huweza pia kutokea kwenye viambishi-awali vya nomino. Jedwali Na. 3 linaonyesha mifano kadhaa kutoka lugha hizo.

Jedwali Na. 3: Irabu ndefu na fupi kwenye viambishi-awali vya baadhi ya nomino za ekiKwaya [EJ251] na eciRuuri [EJ253]

Ngeli	Kiambishi-awali na shina la neno			
	Irabu fupi	**Fasili**	**Irabu ndefu**	**Fasili**
5	<***ri***-*taama*>	kondoo	<***rii***-*táma*>	shavu
	<***ri***-*kééne*>	tegu	<***rii***-*débhe*>	debe
	<***ri***-*siína*>	jina	<***rii***-*sína*>	shina
	<***ri***-*tooke*>	mgomba	<***rii***-*toko*>	shimo
	<***ri***-*gúúwa*>	muwa	<***rii***-*gúwa*>	mfupa

Chanzo: Kiraka (2010); Massamba (2005)

Kutsch Lojenga (2007) anaeleza nadharia-tete mojawapo inayodai kuwa kutokea kwa irabu ndefu kwenye viambishi-awali au viambishi-awali-vitangulizi vya baadhi ya nomino za ishiMalila [M24] za ngeli ya 5, ngeli ya 9 na ngeli ya 10 kunaweza kusababishwa na urefushaji irabu unaofanywa ili kupata maumbo ya nomino yenye mora nne au mora tatu ili maumbo hayo yaweze kutangamana na ruwaza za toni zilizopo katika lugha hiyo.

Inavyoonekana, hali sawa na ya ishiMalila ndiyo hutokea pia kwenye nomino za lugha ya ekiKwaya [EJ251] na eciRuuri [EJ253]. Tumeona kwenye Jedwali Na. 3 kuwa baadhi ya nomino za ngeli ya 5 za ekiKwaya na eciRuuri nazo zina viambishi-awali vyenye irabu fupi na irabu ndefu. Nomino za ngeli hii hazina viambishi-awali-vitangulizi, tofauti na nomino za ngeli zingine za lugha hizi. Kwa sababu hiyo, inaweza kudaiwa kuwa irabu ndefu hutokea katika viambishi-awali hivi kutokana na mchakato wa urefushaji irabu unaofanywa ili kufidia urefu wa irabu ya kiambishi-awali-kitangulizi iliyotoweka kwa sababu fulani. Pengine, urefushaji huo hufanywa ili kuyafanya maumbo ya nomino hizo yawe na idadi ya mora inayotangamana na ruwaza za toni zinazotokea kwenye sehemu ya kiambishi-awali-kitangulizi na kiambishi-awali katika nomino za lugha hizi.

Lugha hizi za Kibantu zilizotolewa mifano hapa ni lugha-toni. Hata hivyo, inajulikana kuwa Kiswahili si lugha-toni (Nurse & Philippson, 2014). Na kama Kiswahili si lugha-toni, je, kuna uwezekano wowote wa ruwaza za toni kuathiri urefu wa irabu za viambishi-awali vya baadhi ya nomino zake kama ilivyo kwa baadhi lugha za Kusini-Magharibi mwa Tanzania na zile za eneo la Maziwa Makuu? Au, je, kuna hali nyingine inayosababisha kutokea kwa irabu ndefu katika viambishi-awali vya baadhi ya nomino zake? Kwa mantiki hiyo, utafiti ulifanywa ili kubaini sababu ya kutokea kwa hali hii.

Kiunzi cha Dhana cha Utafiti

Uchanganuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kwa kuongozwa na dhana tatu za kiisimu. Dhana ya kwanza ni *urefu*. Kifonetiki, *urefu* hurejelea wakaa wa sauti au kitamkwa, ilhali kifonolojia, hurejelea nyakaa za sauti na silabi pindi zinaposababisha tofauti kiisimu (Crystal, 2008). Kwa upande wake, Trask (1996) anafafanua dhana hiyo kwa kusema kuwa *urefu* hurejelea wakaa wa kutamkwa kwa silabi, au irabu, au irabu-unganifu, ambao huchukuliwa kuwa ni sifa ya kifonolojia. Utafiti huu ulichunguza dhana ya *urefu* kwenye viambishi-awali vya nomino za Kiswahili ili kubainisha wakaa wake. Kubainishwa kwa wakaa wa vipashio hivyo, hususani urefu wa irabu zake, kulisaidia kujua iwapo kiambishi-awali kinachohusika kina irabu fupi au irabu ndefu.

Dhana ya pili iliyoongoza uchanganuzi wa data zilizokusanywa kwa ajili ya utafiti huu ni dhana ya *urefushaji*. Trask (1996) anasema kuwa *urefushaji* ni mchakato wowote wa kifonetiki au kifonolojia unaoongeza wakaa wa kipande-sauti ambacho, mara nyingi, huwa irabu. Utafiti huu ulichunguza vipashio mbalimbali vinavyounda nomino za Kiswahili ili kujua kama

vinahusiana kwa namna inayoweza kurefusha irabu za viambishi-awali vya nomino hizo.

Zaidi ya dhana hizo, dhana ya tatu iliyoongoza uchanganuzi wa data za utafiti huu ni *ufupishaji*. *Ufupishaji* ni mchakato wowote wa kifonolojia unaosababisha kipande-sauti kirefu kupoteza urefu wake (Trask, 1996). Hali kadhalika, utafiti huu ulichunguza vipashio mbalimbali vinavyounda nomino za Kiswahili ili kujua kama vinahusiana kwa namna inayoweza kufupisha irabu za viambishi-awali vya nomino hizo.

Methodolojia

Utafiti huu ulitumia mbinu ya usampulishaji sinasibu na usampulishaji nasibu katika kuteua sampuli iliyotoa data za utafiti huu. Sampuli sinasibu ilitumiwa kupata data zilizokusanywa kutoka kwenye maandiko na sampuli nasibu ilitumiwa kupata data za uwandani.

Data zilizotolewa kwenye maandiko zilikusanyiwa katika Chuo Kikuu cha Dodoma kwa mbinu ya upitiaji nyaraka, kutoka kwenye sampuli sinasibu iliyoundwa na *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (BAKITA, 2017), *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (BAKIZA, 2015), na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2014). Data hizo zilikuwa nomino za Kiswahili zilizoingizwa kama vidahizo kwenye kamusi hizo, ambapo viambishi-awali vya nomino hizo vilikuwa irabu au vilijumuisha irabu.

Data za uwandani zilikusanywa kwa mbinu ya usaili kutoka kwa wasemaji wa Kiswahili wa Shehia ya Malindi na Shehia ya Shangani, eneo la Mji Mkongwe, Wilaya ya Mjini Unguja, Zanzibar. Wasemaji hao walisailiwa ili kupata matamshi ya nomino hizo. Matamshi yao yalirekodiwa kwenye

kinasa-sauti na kuchakatwa maabarani kwa kutumia programu ya *Speech Analyzer* ili kubainisha nyakaa za irabu zinazotokea kwenye viambishi-awali vya nomino za Kiswahili. Hatimaye, data hizo zilichanganuliwa kwa kutumia fasili ya dhana ya *urefu*, *urefushaji* na *ufupishaji* ili kubainisha sababu inayofanya viambishi-awali vya baadhi ya nomino za lugha hii kusikika vikiwa na irabu ndefu ilhali nomino zingine zinazobeba kiambishi-awali kilekile zikisikika zikiwa na irabu fupi kwenye kiambishi-awali hichohicho. Kipengele kinachofuata kinawasilisha matokeo ya uchanganuzi huo.

Matokeo ya Utafiti

Uchanganuzi wa matamshi ya wasemaji wa Kiswahili yaliyokusanywa kwa ajili ya utafiti huu unaonyesha kuwa baadhi ya nomino za Kiswahili zina irabu ndefu kwenye viambishi-awali vyake, irabu ambazo hazitokani na kuungana kwa irabu kwenye mipaka ya mofimu, wala kuchombezwa na milolongo ya konsonanti, kama vile milolongo ya nazali na konsonanti au milolongo ya konsonanti halisi. Jedwali Na. 4 linaonyesha baadhi mifano ya nomino hizo.

Jedwali Na. 4: Nomino za Kiswahili zenye irabu ndefu kwenye viambishi-awali zisizotokana na kuungana kwa irabu, wala milolongo ya konsonanti

Chanzo: Data za maandikoni na uwandani (2022)

Ngeli	**Kiambishi-awali**	**Nomino yenye irabu ndefu ya kiambishi-awali**	**Fasili**
1	<mu->	<m**u** + (w)i> → <m**u:**(w)i>	mwovu, mbaya
		<m**u** + ki> → <m**u:**ki>	mtu mwenye fedha nyingi
2	<wa->	<w**a** + tu> → <w**a:**tu>	wingi wa nomino *mtu*
		<w**a** + ki> → <w**a:**ki>	wingi wa nomino *mu:ki*
3	<mu->	<m**u** + wa> → <m**u:**wa>	mmea utoao maji matamu ya sukari
		<m**u** + o> → <m**u:**o>	fimbo yenye ncha ya chuma
		<m**u** + ye> → <m**u:**ye>	mvuke
		<m**u** + ta> → <m**u:**ta>	ndoa ya mkataba wa muda mfupi
4	<mi->	<m**i** + wa> → <m**i:**wa>	wingi wa nomino *mu:wa*
		<m**i** + o> → <m**i:**o>	wingi wa nomino *mu:o*
		<m**i** + ye> → <m**i:**ye>	wingi wa nomino *mu:ye*
		<m**i** + ta> → <m**i:**ta>	wingi wa nomino *mu:ta*
6	<ma->	<m**a** + ji> → <m**a:**ji>	kiowevu cha kunywa, kupikia, n.k.
7	<ki->	<k**i** + mya> → <k**i:**mya>	hali ya kutokuweko sauti au kelele
		<k**i** + nu> → <k**i:**nu>	chombo cha kutwangia nafaka
		<k**i** + nyume> → <k**i:**nyume>	jambo lenye kukinzana na jingine
		<k**i** + sa> → <k**i:**sa>	masimulizi ya kubuni
		<k**i** + tu> → <k**i:**tu>	chochote kiwezacho kushikika, kuonekana, kuhisika, n.k.
		<k**i** + za> → <k**i:**za>	giza nene sana
8	<vi->	<v**i** + nu> → <v**i:**nu>	wingi wa nomino *ki:nu*
		<v**i** + nyume> → <v**i:**nyume>	wingi wa nomino *ki:nyume*
		<v**i** + sa> → <v**i:**sa>	wingi wa nomino *ki:sa*
		<v**i** + ta> → <v**i:**ta>	mapigano ya silaha
		<v**i** + tu> → <v**i:**tu>	wingi wa nomino *ki:tu*
11/14	<u->	<**u** + di> → <**u:**di>	magome ya msandali yatumiwayo kufukizia
		<**u** + ki> → <**u:**ki>	asali
16	<pa->	<p**a** + mo:ja> → <p**a:**mo:ja>	kwa wakati mmoja, kwa kujumuika

Katika utamkaji wa kawaida, irabu fupi za Kiswahili hutamkwa kwa wakaa wa wastani wa sekunde 0.1, ilhali wakaa wa wastani wa kutamka irabu ndefu ni maradufu yake, yaani sekunde 0.2. Tofauti ya wakaa wa irabu ndefu za viambishi-awali hivyo inaweza kusikika vizuri kwa kulinganisha mapigo ya sauti za silabi za nomino hizo na yale ya silabi zinazofanana nazo, lakini zenye irabu fupi, kwenye jozi za nomino zilizopo katika Jedwali Na. 5.

Jedwali Na. 5: Nomino zenye viambishi-awali vyenye irabu ndefu na nomino zenye viambishi-awali vyenye irabu fupi

Irabu ndefu katika k.a.[1]	**Fasili**	**Irabu fupi katika k.a.**	**Fasili**
<m**u:**wi>	mwovu, mbaya	<m**u**pi>	kiulizi cha sehemu ya ndani ya tukio
<m**u:**ki>	mtu mwenye fedha nyingi	<ny**u**ki>	mdudu anayetengeneza asali
<wa:tu>	wingi wa nomino *mtu*	<w**a**fu>	watu waliokufa
<w**a:**ki>	wingi wa nomino *mu:ki*	<w**a**ke>	wanawake walioolewa
<mu:wa>	mmea utoao maji matamu ya sukari	<m**u**me>	bwana
<m**u:**o>	fimbo yenye ncha ya chuma	<ng**u**o>	vazi la kusitiri viungo
<m**u:**ye>	mvuke	<m**u**me>	mwanamume aliyeoa
<m**u:**ta>	ndoa ya mkataba wa muda mfupi	<m**u**da>	kipindi fulani cha wakati
<m**i**:wa>	wingi wa nomino *mu:wa*	<m**i**to>	makorongo yenye maji yatiririkayo
<m**i:**o>	wingi wa nomino *mu:o*	<m**i**a>	idadi ya vitu kumi katika mafungu kumi
<m**i:**ye>	wingi wa nomino *mu:ye*	<m**i**ye>	mimi
<m**i:**ta>	wingi wa nomino *mu:ta*	<m**i**ti>	mimea yenye shina gumu
<m**a:**ji>	kiowevu kutumiwacho kunywa, kupikia, n.k.	<m**a**we>	vipande vidogo vya mwamba
<k**i:**na>	urefu wa kwenda chini ardhini, majini/silabi za sauti za namna moja	<k**i**la>	bila ya kubaki

[1] Kiambishi awali

Irabu ndefu katika k.a.[1]	**Fasili**	**Irabu fupi katika k.a.**	**Fasili**
	zitokeazo baada ya kila mizani kadhaa		
<k**i:**mya>	hali ya kutokuweko sauti au kelele	<k**i**chwa>	sehemu ya mwili yenye ubongo
<k**i:**nu>	chombo cha kutwangia nafaka	<k**i**nywa>	kiungo ambacho ndani kuna ulimi, meno, n.k.
<k**i:**nyume>	jambo lenye kukinzana na jingine	<k**i**nyemi>	kitu kinachopendeza
<k**i:**sa>	masimulizi ya kubuni	<k**i**su>	kifaa cha chuma au bati chenye makali
<k**i:**tu>	chochote kiwezacho kushikika, kuonekana, kuhisika, n.k.	<k**i**to>	jiwe la thamani, k.v. almasi, lulu
<k**i:**za>	giza nene sana	<k**i**ti>	kifaa cha kukalia
<v**i:**na>	wingi wa nomino *ki:na*	<v**i**le>	wingi wa kiwakilishi onyeshi *kile*
<v**i:**nu>	wingi wa nomino *ki:nu*	<v**i**nywa>	wingi wa nomino *kinywa*
<v**i:**nyume>	wingi wa nomino *ki:nyume*	<v**i**nyama>	vipande vidogo vya nyama
<v**i:**sa>	wingi wa nomino *ki:sa*	<v**i**su>	wingi wa nomino *kisu*
<v**i:**ta>	mapigano ya silaha	<v**i**ti>	wingi wa nomino *kiti*
<v**i:**tu>	wingi wa nomino *ki:tu*	<v**i**to>	wingi wa nomino *kito*
<**u:**di>	magome ya msandali yatumiwayo kufukizia	<**u**te>	majimaji mazito yanayoteleza
<**u:**ki>	asali	<**u**ke>	tupu ya mbele ya mwanamke
<p**a:**mo:ja>	kwa wakati mmoja, kwa kujumuika	<p**a**tupu>	pasipo na kitu

Chanzo: Data za maandikoni na uwandani (2022)

Katika Jedwali Na. 4 na Jedwali Na. 5, inaonekana kuwa karibu viambishi-awali vyote vyenye irabu ndefu hutokea kwenye silabi ya pili kutoka mwishoni mwa neno. Ifahamike kuwa nafasi hiyo ya silabi katika neno hudaiwa kurefusha irabu katika lugha nyingi za Kibantu za Mashariki na za

Kusini zilizopoteza sifa ya kutofautisha maana za maneno kwa kutumia urefu wa irabu. Lugha mojawapo yenye sifa hiyo ni Chichewa [N31b] (Hyman, 2014). Hali hiyo ya baadhi ya lugha za Kibantu kurefusha irabu ya silabi ya pili kutoka mwisho wa neno inaweza kudhaniwa na baadhi ya watu kuwa ndiyo husababisha kuwapo kwa irabu ndefu katika viambishi-awali vya maneno kama hayo yaliyo katika majedwali na maneno mengine yanayofanana nayo.

Hata hivyo, utafiti umeonyesha kuwa Kiswahili hakijapoteza sifa ya kutofautisha maana za maneno kwa kutumia urefu wa irabu (Kiraka, 2013). Kwa sababu hiyo, lugha hii si mojawapo ya lugha zilizotajwa na Hyman (2014). Aidha, kuwapo kwa nomino <ki:nyume>, <vi:nyume>, na <pa:mo:ja> katika majedwali hayo—nomino ambazo irabu ndefu katika viambishi-awali vyake hutokea katika silabi ya tatu kutoka mwisho wa neno—kunafutilia mbali uwezekano wa irabu ndefu za viambishi-awali vya nomino za Kiswahili kutokea kwa sababu tu ya kurefushwa na nafasi ya viambishi-awali hivyo katika neno. Sasa basi, kama nafasi ya pili kutoka mwisho wa neno nayo haielekei kuchombeza kutokea kwa irabu ndefu kwenye nomino za Kiswahili, je, ni kwa nini irabu ndefu hutokea katika viambishi-awali vya nomino hizo za Kiswahili?

Uchunguzi unaonyesha kuwa lugha ya Kiswahili haina idadi kubwa ya nomino zenye irabu ndefu katika viambishi-awali. Kwa hakika, hakuelekei kuwa na nomino zingine nyingi zenye irabu ndefu za viambishi-awali zisizotokana na kuungana kwa irabu mbili katika mipaka ya mofimu, wala nomino zenye irabu ndefu za viambishi-awali zisizochombezwa na milolongo ya konsonanti, zaidi ya zile zilizotajwa katika Jedwali Na. 4. Idadi hii ndogo ya nomino za aina hiyo, na ukweli kuwa Kiswahili si lugha-

toni, unaweza kuwafanya baadhi ya watu kudhani kuwa nomino hizo ziliingia katika lugha hii kwa kutoholewa kutoka lugha zingine za Kibantu zenye toni, k.v. ekiKwaya [EJ251], eciRuuri [EJ253], na ishiMalila [M24].

Hoja hiyo inaweza kuwa na ukweli kwa kiasi fulani. Lugha ya Kiswahili inaendelea kutohoa maneno mengi—hususani nomino na vitenzi—kutoka lugha mbalimbali za Kibantu, zikiwamo lugha-toni. Nazo nomino zinazotoholewa kutoka lugha hizo za Kibantu zinaweza kuwa na irabu ndefu kwenye viambishi-awali na kusababisha Kiswahili kurithi irabu hizo ndefu kwenye viambishi-awali. Hata hivyo, tunaweza kujiuliza: Je, nomino hizi za Kiswahili, katika Jedwali Na. 4, zenye irabu ndefu katika viambishi-awali, zinaweza kuwa zimetoholewa kutoka lugha zingine za Kibantu, au zisizo za Kibantu, zenye toni?

Si rahisi kusema iwapo kila nomino ya Kiswahili iliyopo kwenye Jedwali Na. 4 imetoholewa kutoka lugha zingine za Kibantu, au zisizo za Kibantu, zenye toni. Aidha, ikiwa zimetoholewa kutoka lugha hizo zenye toni, si rahisi pia kusema kuwa hiyo ndiyo sababu inayozifanya nomino hizo kuwa na viambishi-awali vyenye irabu ndefu isiyotokana na kuungana kwa irabu kwenye mipaka ya mofimu, wala viambishi-awali vyenye irabu ndefu zisizotokana na kurefushwa na milolongo ya konsonanti.

Tukichunguza kwa makini nomino za Kiswahili zenye irabu ndefu katika viambishi-awali katika Jedwali Na. 4, tunaona kuwa nomino hizo ni aina ya msamiati uitwao msamiati msingi wa lugha. Msamiati msingi huchukuliwa kuwa na kawaida ya kutobadilikabadilika katika lugha yoyote. Msamiati huu huhusu maneno yanayotaja viungo vya mwili (k.v. mgongo, mguu, kichwa), maumbile asilia ya ulimwengu (k.v. mwezi, jua, upepo), na

matendo asilia (k.v. kula, kucheka, kulia) (Massamba, 2007). Jedwali Na. 6 lina nomino kutoka katika jedwali hilo zinazoelekea kuwa sehemu ya msamiati msingi wa Kiswahili.

Jedwali Na. 6: Msamiati msingi wa Kiswahili wenye irabu ndefu katika viambishi-awali

Msamiati msingi wa Kiswahili wenye irabu ndefu katika k.a.	**Fasili**
<w**a:**tu>	wingi wa nomino *mtu*
<m**a:**ji>	kiowevu cha kunywa, kupikia, n.k.
<k**i:**nyume>	jambo lenye kukinzana na jingine
<k**i:**tu>	chochote kiwezacho kushikika, kuonekana, kuhisika, n.k.
<k**i:**za>	giza nene sana
<v**i:**nyume>	wingi wa nomino *ki:nyume*
<v**i:**tu>	wingi wa nomino *ki:tu*
<p**a:**mo:ja>	kwa wakati mmoja, kwa kujumuika

Chanzo: Data za maandikoni na uwandani (2022)

Inavyoonekana, msamiati huu si mgeni katika lugha ya Kiswahili. Haukutoholewa kutoka lugha zingine za Kibantu, wala lugha nyingine za kigeni, bali ulichimbuka kutoka lugha iliyozaa lugha ya Kiswahili. Maumbo yake yanafanana na yale ya ‘visawe’ vyake vilivyoundilizwa vya lugha ya Mame-Bantu, lugha ambayo ni chimbuko la Kiswahili na lugha zingine za Kibantu. Jedwali Na. 7 linaonyesha mifano ya visawe unde vya baadhi ya maneno hayo kama yalivyokuwa katika Mame-Bantu.

Jedwali Na. 7: Kufanana kwa maumbo ya msamiati msingi wa Kiswahili na Mame-Bantu

Sarufi	Msamiati msingi wa Kiswahili wenye irabu ndefu katika k.a.	Msamiati msingi wa Mame-Bantu iliyozaa Kiswahili
Ngeli ya 1 / 2	<mtu / w**a:**tu>	**mʊ=ntʊ / *ba=ntʊ*
Ngeli ya 6	<m**a:**ji>	**ma=jíjI*
Ngeli ya 7 / 8	<k**i:**tu / v**i:**tu>	**kI=ntʊ / *bI=ntʊ*
	<k**i:**za>	**=yid-*
Tarakimu	<m**o:**ja>	**=moi / *=moti*

Chanzo: Schadeberg (2014); Nurse & Philippson (1975)

Inajulikana kuwa Mame-Bantu ilikuwa lugha-toni (Kisseberth & Odden, 2014), na Kiswahili kilirithi msamiati wake mwingi kutoka lugha hiyo. Kwa vile baadhi ya lugha za Kibantu zenye toni, k.v. ishiMalila (M24), hurefusha irabu za viambishi-awali vya nomino ili kuwezesha ruwaza za toni za lugha hizo kujitokeza katika nomino hizo, mabunio yetu ni kwamba, wakati lugha ya Kiswahili nayo ilipokuwa haijapoteza ruwaza zake za toni ilizozirithi kutoka lugha ya Mame-Bantu, ilikuwa ikirefusha irabu za viambishi-awali vya baadhi ya nomino zake ili kuwezesha ruwaza hizo za toni kujitokeza katika nomino hizo. Baadaye, lugha ya Kiswahili ilipobadilika na kupoteza ruwaza zake za toni, irabu ndefu za viambishi-awali vya baadhi ya nomino hizo zilizorefushwa awali ili kuwezesha ruwaza za toni kujitokeza ziliendelea kutokea kwenye viambishi-awali hivyo licha ya kutoweka kwa toni zilizochombeza kurefushwa kwake. Hali hiyo ndiyo inayofanya baadhi ya nomino za lugha hii ziendelee kuwa na viambishi-awali vyenye irabu ndefu zisizotokana na kuungana kwa irabu mbili katika mipaka ya mofimu, wala zisizochombezwa na milolongo ya

konsonanti. Inavyoonekana, kuwapo kwa kundi hili dogo sana la nomino za lugha hii zenye viambishi-awali vyenye irabu ndefu ni ushahidi mmojawapo wa kuwapo kwa mabadiliko ya kihistoria yaliyotokea katika lugha hii yanayoashiria kuwa Kiswahili kilichimbuka kutoka lugha ya Mame-Bantu, nacho kilikuwa na ruwaza za toni, nayo mabaki yake ndiyo haya.

Hitimisho

Katika makala hii, imeelezwa kuwa nomino za Kiswahili, kama zilivyo nomino nyingi za lugha za Kibantu, huundwa na sehemu mbili, yaani shina la nomino na kiambishi cha nomino, kiambishi ambacho, kwa kawaida, ni kiambishi-awali. Uchunguzi wa matamshi ya nomino za lugha hii umeonyesha kuwa kiambishi-awali kilekile kinapoambatishwa kwenye shina la nomino fulani kinaweza kusikika kikitamkwa kwa wakaa mfupi, lakini kiambishi-awali hichohicho kinapoambatishwa kwenye shina la nomino zingine, husikika kikitamkwa kwa wakaa mrefu. Nomino nyingi za Kiswahili zina viambishi-awali vyenye irabu fupi. Hata hivyo, kuna kundi dogo tu la nomino za lugha hii ambazo viambishi-awali vyake vina irabu ndefu. Je, kwa nini hali hii hutokea?

Imeelezwa kuwa irabu ndefu zinaweza kutokea kwenye viambishi-awali vya nomino za Kiswahili kutokana na kuungana kwa irabu ya kiambishi-awali na ile inayopakana nayo kwenye shina la nomino, au kutokana na milolongo ya konsonanti halisi au milolongo ya nazali na konsonanti kurefusha irabu ya kiambishi-awali. Hata hivyo, nomino zilizochunguzwa, zenye viambishi-awali vyenye irabu ndefu, hazina milolongo ya konsonanti, wala irabu mbili zinazokabiliana kwenye mipaka ya mofimu. Kwa mantiki

hiyo, kuna mchakato mwingine unaosababisha kutokea kwa irabu ndefu kwenye viambishi-awali vya nomino hizo za Kiswahili.

Uchunguzi zaidi umeonyesha kuwa kuwapo kwa irabu ndefu katika viambishi-awali vya baadhi ya nomino za Kiswahili kunaweza kuwa kunasababishwa na ruwaza za toni. Inajulikana kuwa lugha ya Kiswahili imeshapoteza ruwaza zake za toni ilizozirithi kutoka lugha ya Mame-Bantu. Na kwa sababu hiyo, inaweza kufikiriwa kuwa toni haiwezi kurefusha irabu za viambishi-awali vya nomino za lugha hii. Badala yake, imedhaniwa, katika utafiti huu, kuwa lugha ya Kiswahili nayo ilipokuwa na ruwaza za toni, ilikuwa ikirefusha irabu za viambishi-awali vya baadhi ya nomino zake, kama zifanyavyo baadhi ya lugha za Kibantu. Baada ya kupoteza ruwaza hizo, baadhi ya nomino za Kiswahili ziliendelea kutumia irabu hizo ndefu kwenye viambishi-awali vyake. Hivyo, kuwapo kwa nomino hizi zenye viambishi-awali vyenye irabu ndefu katika Kiswahili kunaashiria kuwa lugha hii nayo ilikuwa lugha-toni.

Marejeleo

Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (Chapa ya 3). Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) (2015). *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (Chapa ya pili). Nairobi: Oxford University Press.

Crystal, D. (2008). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics* (6th Ed.). Malden, MA: Blackwell Publishing.

Hyman, L.M. (2014). Basaá (A43). Katika Nurse, D. & Philippson, G. (Wah.). *The Bantu Languages* (kur. 257-282). London: Routledge.

Heine, B. (1982). African Noun Class Systems, in H. Seiler and C. Lehmann (eds). *Apprehension sprachliche Erfassen von Gegenständen. Vol 1*. Tübingen Gunter Narr Verlag, 189-216.

Katamba, F. (2014). Bantu Nominal Morphology. Katika Nurse, D. & Philippson, G. (Wah.). *The Bantu Languages* (kur. 103-120). London: Routledge.

Kiraka, P. (2010). "Kamusi ya Nomino na Vitenzi vya EkiKwaya". Kitabu cha mazoezi kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kozi ya *Leksikografia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kiraka, P. (2013). *Urefu, Urefushaji na Ufupishaji wa Irabu katika Kiswahili Sanifu* (Tasnifu ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Kisseberth, C. & Odden, D. (2014). Tone. Katika Nurse, D. & Philippson, G. (Wah.). *The Bantu Languages* (kur. 59-70). London: Routledge.

Kutsch Lojenga, C. (2007). Minimality and Morae in Malila (M.24). Katika Payne, D.L. & Peña, J. (Wah.). *Selected Proceedings of the 37th Annual Conference on African Linguistics* (kur. 77-87). Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project. Inapatikana katika www.lingref.com, document #1597.

Massamba, D.P.B. (2007). *Kiswahili Origins and the Bantu Divergence-Convergence Theory*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam.

Massamba, D.P.B. (2005). *Kamusi ya ciRuuri-Kiswahili-Kiingereza*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nurse, D. & Philippson, G. (1975). Tanzania Language Survey Data. Mswada wa orodha za maneno, haujachapishwa.

Nurse, D. & Philippson, G. (2014). Introduction. Katika Nurse, D. & Philippson, G. (Wah.). *The Bantu Languages* (kur. 1-12). London: Routledge.

Schadeberg, T.C. (2014). Derivation. Katika Nurse, D. & Philippson, G. (Wah.). *The Bantu Languages* (kur. 71-120). London: Routledge.

Steere, E. (1943). *A Handbook of the Swahili Language as Spoken at Zanzibar* (4th ed.). London: Society for Promoting Christian

Knowledge.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la tatu). Nairobi: Oxford University Press.

Trask, R.L. (1996). *A Dictionary of Phonetics and Phonology*. London: Routledge.